# SAUTI YA TSC

TOLEO NA.14 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) APRILI 2022

# TSC YAANIKA MAFANIKIO YAKE, MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN MADARAKANI

1. *Walimu 126,346 wapandishwa vyeo*
2. *Walimu 11,363 wabadilishiwa kazi/ cheo*
3. *Walimu 6,963 wasajiliwa*
4. *Walimu 6,767 wathibitishwa kazini*
5. *Walimu 1,336 wapewa vibali vya kustaafu*
6. *Majalada 132 ya Pensheni, Mirathi na Mikataba yashughulikiwa*
7. *Mashauri 692 yahitimishwa*
8. *Rufaa 191 zahitimishwa*
9. *Pikipiki 74 zanunuliwa na kukabidhiwa wilayani*
10. *Ujenzi wa Ofisi ya TSC Makao Makuu waanza.*



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

# TUMSAIDIE RAIS SAMIA SULUHU HASSAN ILI ALETE MAENDELEO ZAIDI KWA WATANZANIA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ametimiza mwaka mmoja tangu aingie madarakani baada ya aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Mhe. John Joseph Pombe Magufuli kufariki dunia akiwa madarakani Machi 17, 2021.

Katika kipindi kifupi cha uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan sote tumeshuhudia hatua kubwa ya kimaendeleo iliyopigwa katika sekta mbalimbali jambo ambalo limewafanya watanzania kuendelea kuwa na imani zaidi na uongozi wake.

Kwa hapa hatuwezi kuyataja mafanikio yote yaliyopatikana katika uongozi wa Rais Samia, lakini tunaweza kujikubusha mambo makubwa mawili aliyoyafanya kwa walimu ambayo yataendelea kukumbukwa hata na vizazi vijavyo.

Jambo la kwanza ni uamuzi wake wa kumaliza kero sugu ya walimu kukaa muda mrefu bila kupata haki yao ya kupandishwa vyeo. Kila mmoja wetu anatambua kwamba suala la kutopandishwa vyeo lilikuwa ni kilio kikubwa kwa walimu na wengine walikuwa wamefikia hatua ya kukata tamaa na kuanza kusua sua katika kutimiza majukumu yao ya kufundisha wanafunzi. Baada ya uamuzi huo, TSC ilipandisha walimu ambao ndio waliokuwa na sifa kwa mujibu wa taratibu na mishahara yao ilibadilishwa kwa wakati.

Jambo la pili ni kuweka mazingira mazuri kwa walimu kufundisha na wanafunzi kupata elimu kwa kuboresha miundombinu mbalimbali shuleni ikiwemo ujenzi wa zaidi ya madarasa 15,000 nchi nzima. Hii imesaida kupunguza mlundikano wa wanafunzi darasani na kumpa mwalimu fursa ya kufundisha wanafunzi katika mazingira bora zaidi. Jambo jilo limeleta heshima kwa walimu na kuongeza morali ya utendaji kazi kitu ambacho kinaifanya sekta ya elimu kuendelea kufanya vizuri.

Ukweli ni kwamba Rais Samaia Suluhu Hassan ana maono na malengo makubwa zaidi katika kuendelea kuboresha maisha ya Watanzania katika njanja mbalimbali, na malengo hayo yatafikiwa tu endapo kila mmoja wetu atatimiza wajibu wake ipasavyo katika eneo lake la kazi.

Hivyo, ni wito wetu kwa kila mtendaji ndani na nje ya utumishi wa umma kuhakikisha anatekeleza majukumu yake kwa bidii, weledi, ubunifu na uadilifu zaidi ili malengo ya Rais Samia Suluhu Hassan yaweze kutimizwa kwa wananchi.

## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina Nkwama


**Wajumbe**
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya

**Mhariri Mkuu**
Gerard Chami

**Mhariri**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

## KATUNI




**Wasiliana nasi kwa Simu:** +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***

# TSC YAANIKA MAFANIKIO YAKE, MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN MADARAKANI

**Na. Mwandishi Wetu - Dodoma**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainiswa kwenye Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015. TSC ni Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari walio kwenye Utumishi wa Umma, Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, miongoni mwa majukumu ya TSC ni kusimamia masuala yanayohusu ajira ya Mwalimu ambayo ni kusajili na kutoa barua za ajira rasmi; kuthibitisha kazini; kupandisha vyeo; kubadilisha kazi/cheo waliojiendeleza; kuandaa Tange, kupitisha na kuratibu maombi ya kuajiriwa upya kwenye Utumishi wa Umma.

TSC pia inawajibika kushughulikia mafao ya wastaafu na mirathi ambayo haishughulikiwi na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kukokotoa mafao na kuwasilisha kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Hazina kwa ajili ya uhakiki na malipo.

Jukumu lingine ni kusimamia Maadili na Nidhamu kwa Walimu kwa kuwaelimisha na kuchukua hatua za kinidhamu kwa wanaokiuka Sheria, Kanuni na Maadili ya Utumishi wa Walimu na Utumishi wa Umma.

Sheria hiyo pia imeipa TSC jukumu la kuhakikisha kunakuwa na uwiano sawa katika upangaji wa walimu ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Shule pamoja na kusimamia Programu za Mafunzo ya Walimu Kazini.

Majukumu mengine yanayotekelezwa na ofisi hiyo ni kufanya tafiti kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Utumishi wa Walimu pamoja na kufanya tathmini ya hali ya walimu na kumshauri Waziri anayehusika na mafunzo ya walimu kuhusu idadi, aina ya mafunzo na uhitaji wa walimu nchini.

TSC inatekeleza majukumu haya kupitia Ofisi yake ya Makao Makuu iliyopo mtaa wa Mtendeni jijini Dodoma pamoja na ofisi 139 zilizopo katika kila Wilaya Tanzania Bara na inasimamia walimu 258,291 ambao kati yao Walimu 173,591 ni wa Shule za Msingi na Walimu 84,700 ni wa Shule za Sekondari.

Katika kipindi cha mwaka mmoja tangu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan aingie madarakani baada ya aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Mhe. John Joseph Pombe Magufuli kufariki dunia akiwa madarakani Machi 17, 2021, TSC imeendelea kupata mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa kutoa huduma kwa walimu.

Itakumbukwa kuwa tarehe 1 Mei, 2021 katika sherehe za siku ya wafanyakazi, Mhe. Rais aliwashangaza watanzania wengi hasa pale alipotoa maelekezo kwa watendaji wa Serikali kuwa watumishi wa Umma wenye sifa za kupanda vyeo wapandishwe. Maelekezo hayo yalipokelewa na watumishi wa umma wakiwemo walimu kwa shangwe kwani yaliwafuta machozi ya muda mrefu ya kukaa muda mrefu bila kupandishwa vyeo licha ya kuwa na sifa za kupanda.

Kufuatia agizo hilo la Rais, TSC kupitia Kamati zake za Wilaya ambazo ndizo zenye mamlaka ya kuamua masuala ya Ajira, Nidhamu na Maendeleo ya Walimu zilianza kufanya vikao vya kupandisha vyeo walimu mara moja ambapo ambapo Walimu



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiapishwa kushika nafasi ya Rais mwezi Machi, 2021.*

# TSC YAANIKA MAFANIKIO YAKE, MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN MADARAKANI



*Moja ya Mafunzo ya Kamati za Waliya yaliyowezeshwa kufanyika na Rais Samia Suluhu Hassan*

126,346 walipandishwa vyeo na walimu 11,363 walibadilishiwa kazi/cheo baada ya kujiendeleza.

Ndani ya mwaka mmoja wa Rais Samia, TSC kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) ilifanya kazi ya kukusanya, kuchambua na kuandaa taarifa ya tathimini ya usambazaji na uwiano wa walimu kupitia mfumo wa School Information System (SIS).

Katika kipindi cha mwaka mmoja madarakani, Rais Samia Suluhu Hassan amewezesha walimu 6,963 ambao walikuwa ni ajira mpya katika utumishi wa Umma kusajiliwa na kupatiwa namba za utambulisho (TSC namba) huku jumla ya walimu 6,767 wakithibitishwa kazini baada ya kukidhi vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria.

Sambamba na hilo, Rais Samia amewezesha Makamishna tisa (9) wa Tume pamoja na Wajumbe 164 wa Kamati za TSC ngazi ya wilaya kutoka Kanda ya Kati, Nyanda za Juu Kusini na Mangaribi ikihusisha mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe, Rukwa, Kigoma, Tabora, Katavi, Shinyanga, Dodoma, Singida, Manyara na Iringa kupatiwa mafunzo elekezi ya utekelezaji wa majukumu ya Tume. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuhakikisha Kamati hizo zinakuwa na uelewa wa kutosha ili ziweze kutenda haki na kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria na Kanuni pale zinapotakiwa kuamua masuala mabalimbali ya walimu.

Katika kuhakikisha mafunzo yaliyotolewa yanaleta manufaa katika kushughulikia masuala ya utumishi wa walimu, ufuatiliaji ulifanyika katika Wilaya mbalimbali na kubaini kuwa mafunzo hayo yameleta mabadiliko katika utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Katika kipindi cha mwaka mmoja madarakani, Rais Samia amezewesha walimu 1,336 kupata vibali vya kustaafu kazi ambapo walimu 1,245 walikuwa ni walimu wa shule za misingi na 91 walikuwa ni walimu wa shule za sekondari.

Vilevile, katika kipindi cha mwaka mmoja madarakani, Rais Samia amefanikiwa kushughulikia masuala ya Pensheni, Mirathi na Mikataba ya walimu ambapo majalada 133 ya yalipokelewa na kushughulikiwa kwa kufanyiwa uchambuzi wa nyaraka, ukokotoaji wa hesabu na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na HAZINA kwa ajili ya malipo. Kati ya majalada hayo, majalada 37 yalihusu Mikataba, 13 Pensheni na 83 Mirathi.

Chini ya usimamizi na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, TSC imeandaa Mwongozo kwa ajili ya kuwasidia Wakuu wa Shule kwa nafasi zao za Mamlaka za nidhamu ngazi ya Shule umesaidia kushughulikia masuala ya walimu ngazi ya shule na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa walimu. Mwongozo huo umesambazwa kwa Wakuu wote wa Shule za Msingi na Sekondari.

Katika kipindi cha Machi 2021 hadi Machi, 2022 Rais Samia ameiwezesha TSC kufungua Mashauri ya Nidhamu 1,065 yanayohusu utovu wa nidhamu na katika idadi hiyo mashauri 692 sawa na asilimia 65 ya mashauri yaliyofunguliwa yalishughulikiwa na kuhitimishwa huku Mashauri 373 yakiwa yanaendelea kushughulikiwa.

# TSC YAANIKA MAFANIKIO YAKE, MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN MADARAKANI



*Aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Seikali za Mitaa (TAMISEMI) ambaye kwa sasa ni Waziri wa Afya, Mhe. Ummy Mwalimu (MB) akiwa amekabidhi pikipiki kwa mmoja wa Watumishi wa TSC ngazi ya Wilaya ikiwa ni ishara ya kukabidhi pikipiki 74 kwa ofisi mbalimbali za TSC Wilaya. Tukio hilo lilifanyika Septemba 7, 2021.*




*Baadhi ya pikipiki zilizonunuliwa chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.*

Endapo mwalimu hajaridhika na uamuzi wa shauri lake, Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 imempa haki ya kukata rufaa. Mamlaka ya kwanza ya rufaa ni Kamati ya Wilaya kwa uamuzi uliotolewa na Mkuu wa Shule. Mamlaka ya pili ni Tume Makao Makuu kwa uamuzi uliotolewa na Mamlaka ya Nidhamu ngazi ya Wilaya na Mamlaka ya mwisho ni Rais kwa uamuzi uliotolewa na Tume Makao Makuu. Katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia madarakani, rufaa 216 zilikatwa na kupokelewa TSC Makao Makuu ambapo katika idadi hiyo, rufaa 191 zilihitimishwa.

Rais Samia Suluhu Hassan ameendelea kuiwekea TSC mazingira bora ya utendaji wa kazi kwa kuiwezesha kununua kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za TSC Makao Makuu ambapo kiasi cha shilingi milioni mia tano kilitolewa ili kuanza ujenzi wa ofisi hizo. Aidha, Rais Samia ameelekeza fedha za kuendeleza ujenzi huo ziendelee kutengwa katika bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/2023.

Ukweli ni kwamba hatuwezi kuainisha mafanikio yote ya TSC yaliyotokana na uongozi wa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan lakini jambo lingine ambalo litaendelea kukumbukwa ni kuiwezesha TSC kununua pikipiki 74 kwa ajili ya ofisi za Wilaya. Pikipiki hizo zimesaidia kwa kiasi kikubwa watumishi wa TSC ngazi ya Wilaya kuwafikia walimu na kutatua changamoto mbalimbali kwa wakati.

TSC imedhamiria kutoa huduma bora ili walimu waweze kutimiza wajibu wao wa kuwafundisha wanafunzi kikamilifu, hivyo itaendelea kufanya jitihada mbalimbali ikiwemo matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuhakikisha huduma zinawafikia walimu kwa haraka zaidi.

Rais Samia Suluhu Hassan ameonesha mafanikio makubwa katika kipindi kifupi cha uongozi wake Kwa kushughulikia malamiko mbalimbali ya walimu, moja ya malamiko makubwa ilikuwa ni kutopandishwa vyeo kwa muda mrefu, vilevile Rais Samia ameboresha mazingira ya kufundishia kwa kuongeza vyumba vya madarasa. Kutokana na juhudi hizo, walimu wana wajibu wa kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa moyo wake wa kutanguliza maslahi ya watumishi wa umma. Hivyo ni vyema watumishi wa umma kufanya kazi kwa bidii, ubunifu, weledi na nidhamu ili Tanzania iendelee kuwa na ustawi bora zaidi.

Hongrea sana Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Walimu wana imani kubwa na wewe na wataendelea kukuunga mkono, kazi iendelee.

# MSIWALAZIMISHE WALIMU KUKOPA KWENYE BENKI MNAZOTAKA NYIE: WARIZI BASHUNGWA




**Na. Mwandishi Wetu - Dodoma**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa amewataka Maafisa Utumishi kote nchini kuacha mara moja tabia ya kuwalazimisha walimu kukopa fedha kwenye benki wanazozitaka kinyume na taratibu za kiutumishi.

Katazo hilo amelitoa hivi karibuni jijini Dodoma wakati akitoa taarifa mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani katika kikao kilichowakutanisha Makatibu Tawala wa Mikoa, Viongozi wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya TAMISEMI, Wakurugenzi wa Hamlamshauri pamoja na Waandishi wa Habari.

Waziri huyo alieleza kuwa kuna baadhi ya watumishi wa Halmashauri ambao kwa maslahi yao wenyewe wanawagomea walimu kuwapitishia fomu za kuomba mikopo kwa vile wanataka walimu hao wakakope katika benki wanazotaka maafisa hao.

"Walimu ni watumishi kama walivyo watumishi wengine wana uhuru wa kuamua kwenda kukopa katika benki wanayotaka ilimradi wamezingatia taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Innocent Bashungwa, akizungumza wakati akieleza mafanikio ya mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani kwenye kikao kazi cha Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya TAMISEMI na Waandishi wa Habari kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

# MSIWALAZIMISHE WALIMU KUKOPA KWENYE BENKI MNAZOTAKA NYIE: WARIZI BASHUNGWA



*Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Prof. Riziki Shemdoe, akizungumza kwenye kikao kazi cha Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya TAMISEMI na Waandishi wa Habari kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma ambapo pamoja na mambo mengine kikao hicho kilizungumzia mafanikio ya mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani.*

sheria. Sasa cha kushangaza kuna maafisa utumishi kwenye halmashauri wanawaambia walimu kama wanataka wapitishe fomu zao, lazima wakope kwenye benki flani wanayotaka wao, sasa sijui wana maslahi gani na hizo benki," alisema Bashungwa.

Alifafanua kuwa, moja ya mikakati ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha watumishi wa umma wakiwemo walimu wanafanya kazi katika mazingira bora ikiwa ni pamoja na kupatiwa haki zao za kiutumishi kwa wakati na bila usumbufu.

"Kukopa ni haki ya mtumishi ilimradi amekidhi vigezo, ninataka watumishi wenye tabia ya kuwasumbua walimu kwenye masuala ya mikopo na masuala mengine ya kiutumishi waache tabia hiyo mara moja kwani wanarudisha nyuma juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan na mimi nikiwa msaidizi wake siko tayari kuona hilo linatokea," alisema.

Waziri bashungwa aliitaka pia Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kuhakikisha inawasaidia walimu kutambua na kupata haki zao kwa wakati pamoja na kushughulikia kero na malalamiko yao ili waweze kuwa na moyo wa kuwafundisha wanafunzi kwa bidii zaidi.

"Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan amekwisha tuelekeza kwamba tuiwezeshe Tume ya Utumishi wa Walimu ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kusimamia Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kikamilifu. Hivyo, TSC mna wajibu mkubwa wa kuhakikisha

# MSIWALAZIMISHE WALIMU KUKOPA KWENYE BENKI MNAZOTAKA NYIE: WARIZI BASHUNGWA

masuala ya utumishi wa walimu mnayashughulikia kikamilifu ili wafanye kazi kwa amani," alisema Bashungwa.

Pamoja na hayo, Waziri Bashungwa amewaelekeza Wakurugenzi wa Halmshauri zote nchini kutatua changamoto sugu ya upungufu wa matundu ya vyoo hasa katika shule za msingi badala ya kukaa na kusubiri maelekezo kutoka ngazi za juu bila wao kufanya chochote.

"Tumejengewa madarasa mazuri watoto wetu waweze kusoma bila kubanana hivyo tunasubiri Rais aje aseme na matundu ya vyoo wakati wakurugenzi na na Katibu Tawala mpo," amesema Bashugwa.

Aliongeza kuwa "Sasa wakurugezi kwenye bajeti zenu wekeni kiaumbele na mikakati ya kumaliza tatizo hili, mna mapato mengi ya makusanyo ya ndani, tatueni tatizo hilo la upungufu wa vyoo. Msisubiri vyombo vya habari vije viibue upungufu huo ndipo mchukue hatua," amesema.

Amesema takwimu zinaonyesha upungufu wa matundu ya vyoo kwa shule za msingi nchi nzima ni zaidi ya 200000 huku upungufu wa matundu hayo kwa shuke za sekondari ni 44605.





*Viongozi mbalimbali wakifatilia hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Innocent Bashungwa (hayupo pichani) wakati akieleza mafanikio ya mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani kwenye kikao kazi cha Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya TAMISEMI na Waandishi wa Habari kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*


OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)
1959 - 2021
1
Tunaungana na Watanzania wote katika Kumbukizi ya mwaka moja wa kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania , Hayati John Pombe Joseph Magufuli. Tunatambua mchango wako katika kuwajali na kuwathamini Walimu hadi Serikali kuamua kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) nchini mwaka 2016 ili Walimu wahudumiwe kwa ufanisi zaidi.
"Tutaendelea kutoa huduma bora ili tutimize maono yako katika usimamizi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu nchini"
www.tsc.go.tz
Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

# ZINGATIENI TARATIBU KATIKA KUSHUGHULIKIA MASHAURI YA NIDHAMU YA WALIMU: KATIBU TSC



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akisaini kitabu cha wageni katika ofisi ya TSC Wilaya Songwe wakati wa Ziara yake aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akitoa maelekezo kwa Watumishi wa TSC Wilaya Songwe (hawapo pichani) wakati wa Ziara yake aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.*

**Na Mwandishi Wetu – Songwe**

Kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Sura 448, Ofisi za TSC ngazi ya Wilaya ni Mamlaka ya kushughulikia mashauri ya nidhamu ya walimu pamoja na rufaa za walimu zinazotokana na uamuzi unaofanywa na mamlaka ya kwanza ya nidhamu ambayo ni Wakuu wa Shule.

Uamuzi wa mashauri pamoja na rufaa za walimu unaofikiwa na Kamati za TSC Wilaya unafanyika baada ya hatua mbalimbali zilizowekwa kuzingatiwa, na ili uamuzi uwe wa haki ni lazima hatua zote za shauri zifuate sheria, kanuni na taratibu ili kuepuka makosa yanaweza kuharibu shauri.

Katika kuazimisha mwaka mmoja tangu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan aingie madarakani, Katibu wa TSC, Paulina Nkwama alifanya ziara katika ofisi mbalimbali za TSC



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Songwe, Issa Shemgei Shehagilo akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa ofisi yake kwa Katibu wa TSC (hayupo pichani) katika ofisi za tume hiyo wilani songwe hivi karibuni.*



*Afisa Maadili na Nidhamu wa TSC Wilaya ya Songwe, Leonard Fraiton Mbukwa akitoa taarifa ya masuala ya Nidhamu ya Walimu kwa Katibu wa TSC (hayupo pichani). Alitoa maelezo hayo katika ziara ya Katibu wa TSC aliyoifanya wilani hapo hivi karibuni.*

# ZINGATIENI TARATIBU KATIKA KUSHUGHULIKIA MASHAURI YA NIDHAMU YA WALIMU: KATIBU TSC



*Katibu Muhtasi, Florah Chanda (wa kwanza kushoto) kutoka TSC Makao Makuu akiwaelekeza watumishi wa TSC Wilaya ya Songwe utaratibu wa kuandika barua za Serikali na namna bora ya kutunza nyaraka za ofisi.*

Wilaya ambapo moja ya mabo aliyoyasisitiza kwa watumishi wa TSC ni kuhakikisha wanazingatia taratibu zote katika kushughulikia mashauri ya walimu.

Akiwa wilayani Songwe, Nkwama alisema kuwa katika rufaa zinazokatwa Tume makao Makuu baada ya warufani kutoridhishwa na uamuzi wa TSC ngazi ya Wilaya moja ya mabo yaliyobainika ni kutozingatiwa kwa taratibu kitu ninachosababisha kutotendeka kwa haki.

Alifafanua kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imekusudia kushughulikia masuala ya walimu kwa haki na weledi hivyo ni wajibu wa watumishi wa tume hiyo kuzisoma na kuzielewa sheria na kanuni ili waweze kuzishauri vyema kamati za Wilaya wakati wa kufanya maamuzi ya mashauri ya walimu.

"Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ametuweka ili tumsaidie katika kutekeleza majukumu yanayohusu utumishi wa walimu. Ukiangalia katika kipindi hiki cha mwaka mmoja Rais amefanya mambo mengi ya kuwaletea maendeleo wananchi, hivyo nasisi moja ya maendeleo tunayopaswa kuyafanya katika kuboresha utumishi wa walimu ni kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili tutende haki wakati wote," alisema Nkwama.

"Katika rufaa tunazopokea, tumeona kwamba kuna kutokuzingatiwa kwa sheria na kanuni katika kushughulikia mashauri haya. Na kule Makao Makuu Tume inapitia kila kipengele kwa umakini ili kuona kama kila hatua ilizingatia sheria. Matokeo yake tumekuta warufani wanashinda kutokana na udhaifu katika kuzingatia taratibu uliofanyika huku wilayani. Kosa linaweza kuwepo, lakini ukikosea kuzingatia taratibu kesi yote inaharibika," alisema.

Kiongozi huyo aliendelea kueleza kuwa miongoni mwa



*Maafisa kutoka TSC Makao Makuu walioambatana na Katibu wa TSC katika ziara yake wilayani Songwe wakipitia baadhi ya nyaraka ofisini hapo. Katikati ni Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Maadili na Nidhamu ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Robert Lwikolela.*

# ZINGATIENI TARATIBU KATIKA KUSHUGHULIKIA MASHAURI YA NIDHAMU YA WALIMU: KATIBU TSC

taratibu za kuzingatia ni uandishi wa hati ya mashtaka ambayo inatakiwa kuelezea kwa ufasaha wakati, mahali na namna kosa lilivyotendwa huku ikionesha kosa hilo limekiuka kifungu gani cha sheria/kanuni.

Aidha, endapo shauri limeundiwa kamati ya uchunguzi ni lazima mtuhumiwa apewe wito wa kuhudhuria kwenye kikao cha kamati hiyo, ni lazima uwepo ushahidi kuwa mtuhumiwa amepokea barua ya wito na wakati wa kikao mtuhumiwa apewe nafasi ya kuwahoji mashahidi na kuona nyaraka zote zinazotumia kama ushahidi dhidi yake.

"Kuna changamoto kwenye kuitwa kwa mtuhumiwa kwenye kamati ya uchunguzi, mara nyingi tunaona barua ya wito imeandikwa lakini hatuoni ushahidi wa mtuhumiwa kupokea wito huo. Wengi wanaandika barua ya kumwita mtuhumiwa lakini hawachukui hatu za ziada kuhakikisha barua ya wito inamfikia mhusika," alisema.

Vilevile, aliwataka watumishi hao kuhakikisha wanatunza nyaraka za ofisi vizuri kwa ajili ya kumbukumbu na pale zinapohitajika kwa ajili ya matumizi mengine ziweze kupatikana kwa urahisi ili kusaidia shughuli zingine zinazotegemea




*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Songwe wakati alipofanya ziara wilayani hapo hivi karibuni.*

nyaraka hizo ziweze kufanyika.

"Wote mnajua kwamba mwalimu anapokata rufaa Tume Makao Makuu, kitu cha kwanza tunachofanya ni kuwataka muwasilishe nyaraka zote za shauri hilo, maana hatuwezi kushughulikia rufaa bila kupata nyaraka za shauri kutoka wilayani. Sasa inashangaza unapoagiza nyaraka inachukua miezi nyaraka hazileti, hii siyo sawa hata kidogo, ni lazima tubadilike," alisema.

Naye Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Songwe, Issa Shemgei Shehagilo alisema Wilaya ya Songwe ina jumla ya shule za msingi 56 na za sekondari 11 za Serikali huku ikiwa na jumla ya walimu wa shule za msingi 458 na shule za sekondari 175 wanaohudumiwa na TSC kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya

**"... hatuwezi kushughulikia rufaa bila kupata nyaraka za shauri kutoka wilayani. Sasa inashangaza unapoagiza nyaraka inachukua miezi nyaraka hazileti, hii siyo sawa hata kidogo, ni lazima tubadilike..."**

# ZINGATIENI TARATIBU KATIKA KUSHUGHULIKIA MASHAURI YA NIDHAMU YA WALIMU: KATIBU TSC




*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Songwe pamoja na watumishi wa TSC Makao Makuu walioambatana nae katika ziara aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.*

Utumishi wa Walimu Sura 448.

Akielezea mafanikio ya TSC Wilaya ya Songwe katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan, Shehagilo alisema kuwa mwaka 2020/2021 jumla ya walimu 245 walipandishwa vyeo ambapo katika idadi hiyo walimu 153 ni wa shule za msingi na 92 ni wa sekondari huku walimu 25 wakibadilishiwa kazi/cheo baada ya kujiendeleza kimasomo.

"Tunamshukuru Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa sababu kutokana na maelekezo yake hakuna mwalimu aliyestahili kupandishwa ambaye alisahaulika. Walimu wote 245 tuliowapandisha walibadilishiwa mishahara na kuanza kupokea mishahara ya vyeo vipya ndani ya muda mfupi tofauti na ilivyokuwa siku za nyuma," alisema Shehagilo.

Kwa upande wa nidhamu kwa walimu, Shehagilo alisema kuwa nidhamu ya walimu imeendelea kuwa nzuri kwani kwa mwaka 2020/2021 ofisi hiyo ilikuwa na shauri moja tu na kwa mwaka 2021/2022 kuna mashauri matatu huku akieleza kuwa mafanikio hayo ni kutokana na juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan za kuendelea kuiwezesha TSC kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuwafikia walimu na kuwapatia elimu kuhusu utumishi wao.

"Tumefanikiwa kusambaza vijitabu vya Kanuni za Maadili ya Kazi ya Ualimu kwa shule 56 za msingi na 11 za sekondari. Tumefanya ziara kwenye shule 23, pia tumeendelea kufanya semina na mikutano kwa ajili ya kuwajengea uwezo wakuu wa shule kuhusu majukumu yao wakiwa ni mamlaka ya kwanza ya nidhamu kwa walimu. Vilevie, tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwani kupitia uongozi wake tumefanikiwa kuwafikia walimu 458 na kuwapa elimu juu ya masuala ya utumishi wao," alisema.

Katika ziara hiyo, watumishi wa TSC Songwe walipata fursa ya kukumbushwa masuala mbalimbali ya kiutumishi yakiwemo namna ya kuandika barua za Serikali kwa kuzingatia Miongozo iliyopo, namna ya kutunza nyaraka za ofisi pamoja

# TSC GAIRO YAJIVUNIA KUIMARISHA UHUSIANO NA WADAU WA ELIMU



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Gairo, Juma Eustace akitoa ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya TSC katika Wilaya hiyo wakati jarida hili lilipofika ofisini kwake hivi karibuni.*

**Na Mwandishi wetu - Gairo**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Gairo mkoani Morogoro imeendelea kupiga hatua katika kuimarisha uhusiano na mawasiliano kati yake na wadau wa elimu wilayani hapo kwa lengo la kuendelea kutoa huduma bora kwa walimu.

Kauli hiyo imetolewa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Gairo, Juma Eustace wakati alipotembelewa na jarida hili hivi karibuni kwa lengo la kupata taarifa za utekelezaji wa majukumu ya TSC katika wilaya hiyo.

Kwa mujibu wa Eustace Wilaya hiyo ina Halmashauri moja inayoundwa na kata 18 zenye jumla ya vijiji 50 huku ikiwa na shule za msingi 70 na shule za sekondari 14 za serikali.

Aliendelea kufafanua kuwa Wilaya hiyo ina jumla ya walimu wa shule za msingi 675 na walimu 245 wa shule za sekondari wanaofundisha darasani.

Kuhusu kuendelea kuimarika kwa uhusiano na mawasiliano baina ya TSC na wadau wengine wa elimu, Eustace alisema ofisi yake imekuwa ikikutana mara kwa mara na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Wathibiti Ubora wa Shule, Chama cha Walimu (CWT) na wadau wengine kwa lengo la kujadiliana masuala mbalimbali yanayohusu utumishi wa walimu.

"Katika Wilaya yetu tumeunganisha viongozi mbalimbali wanaoshughulikia masuala ya elimu kwa kutumia kundi la WhatsApp linaloitwa Gairo TSC Working Group ili kupashana habari, kupeana elimu na taarifa mbalimbali zinazohusu masuala ya walimu," alisema Eustace.

Aliongeza kuwa kuwepo kwa uhusiano huo kumesaidia ofisi yake kuendelea kupata heshima na kushirikishwa katika mikutano na matukio mbalimbali yanayotokea wilayani hapo ambapo wanapata fursa ya kuitangaza TSC pamoja na majuku yake.

Kutokana na ukaribu huo, ofisi hiyo imepiga hatua katika kutatua kero mbalimbali za walimu kwa kushirikiana mwajiri kupitia Idara ya Elimu ya Msingi na Sekondari na hivyo kufanya walimu kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kwa kujituma zaidi katika kutoa huduma kwa wanafunzi.

"Kuna mabadiliko makubwa na furaha kwa walimu hasa kwa sababu tunazingatia utu



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Gairo, Juma Eustace (kulia) akizungumza na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami hivi karibuni katika ofisi za TSC Wilaya ya Gairo.*

# TSC GAIRO YAJIVUNIA KUIMARISHA UHUSIANO NA WADAU WA ELIMU



*Mtumishi wa TSC Wilaya ya Gairo, Mawazo Tuliwanje akiwa ofisini kwake.*



*Mtumishi wa TSC Wilaya ya Gairo, John Rweikaza akiwa ofisini kwake.*

wa mtu katika kutatua masuala ya walimu. Ukiangalia Jiografia ya Wilaya yetu, walimu wengi wanatoka mbali kuja hapa kutafuta huduma," alisema.

Aliendelea kufafanua kuwa, "wakati mwingine unaweza kukuta mwalimu ameingia ofisini lakini hayupo katika mwonekano mzuri kutokana na purukushani za njiani. Akija kwetu sisi hatumfokei tunakaa nae kwanza tunaongea nae, tunamsikiliza na kumtia moyo ndipo tuanze kumpa elimu juu ya taratibu za kiutumishi ikiwemo namna ya kuwa na mwonekano nadhifu wa kiutumishi."

"Tunajitahidi kushughulikia shida ya mwalimu siku hiyo hiyo, pale ambapo tunaona suala lake haliwezi kumalizika kwa siku moja, tunachukua mawasiliano yake na punde tunapokalimisha suala husika tunamjulisha, yote hayo ni kwa ajili ya kuhakikisha tunampunguzia gharama ya kuja ofisini mara kwa mara."



*Picha ya pamoja kati ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami (wa pili kutoka kulia) na watumishi wa TSC Wilaya ya Gairo.*

Kuhusu hali ya nidhamu kwa walimu wilayani hapo, kiongozi huyo alisema kuwa walimu wengi wanazingatia sheria na taratibu za utumishi wa walimu na zile za utumishi wa umma kutokana na jitihada zinazofanywa na ofisi yake katika kutoa elimu hivyo, mashauri ya nidhamu yameendelea kupungua.

"Mwaka 2016/17 tuliwafukuza kazi walimu tisa, 2017/18 walifukuzwa watatu, 2018/19 walifukuzwa wawili, 2019/20 walifukuzwa walimu watatu na 2020/21 walifukuzwa kazi walimu 4. Tunasikitika sana kumfukuza kazi mwalimu na tunataka tufike sehemu tusiwe na mwalimu anayefukuzwa kazi wala kufunguliwa shauri la nidhamu," alisema.


OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)
Kuelekea siku ya
Wanawake Duniani
Tunasimamia kikamilifu miiko
na maadili ya kazi ya Ualimu
ili Wanafunzi wa kike waendelee
kufurahia haki ya kupata Elimu
kwa ajili ya ustawi wa Taifa letu
Tujitokeze Kuhesabiwa
Mwl. Paulina Nkwama, ndc
Katibu Ofisi ya Rais - TSC
www.tsc.go.tz
Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

# WATUMISHI TSC WATAKIWA KUACHA MIGOGORO NA MIVUTANO KAZINI INAYOKWAMISHA MALENGO YA SERIKALI YA KUTOA HUDUMA BORA KWA WALIMU

**Na Mwandishi wetu - Momba**

Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wametakiwa kufanya kazi kwa ushirikiano na kuachana na migogoro na mivutano ambayo inakwamisha utekelezaji wa majukumu ya tume hiyo na kusababisha kutofikiwa kwa malengo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan katika kuboresha utumishi wa walimu.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama wakati alipotembelea ofisi za TSC Wilaya ya Momba iliyopo mkoani Songwe kwa lengo la kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya TSC katika wilaya hiyo ikiwa ni mwaka mmoja tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani.

Nkwama alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan ina matarajio kuwa TSC itakuwa suluhisho la changamoto za walimu, hivyo ni lazima kila mtumishi wa tume hiyo afanye kazi kwa bidii, nidhamu, weledi na mshikamano kuku akisisitiza kuwa kamwe hatamvumilia mtumishi atakayekuwa chanzo cha migogoro na mivutano kazini.

"Tumewekwa na Rais ili tuwahudumie wananchi na sisi TSC wananchi wetu ni walimu. Tuna jukumu kubwa sana kwani mwalimu anapoingia kwenye ajira hadi anapohitimisha utumishi wake yupo mikononi mwetu. Sisi tunaweza kumfanya aipende kazi yake au aichukie, awe na nidhamu au mtovu wa nidhamu, atengeneze Taifa bora la kesho au Taifa bovu."

"Hivyo, ili kuweza kuyafanya hayo yote kwa ufanisi ni lazima tuweze kuwajibika ipasavyo. Zipo baadhi ya ofisi zetu ambazo



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Paulina Nkwama akisisitiza jambo katika kikao chake na Watumishi wa TSC wa Wilaya ya Momba (hawapo pichani) hivi karibubuni.*




*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Momba, Juma Seleman (kulia) akitoa maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi yake kwa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu. Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC wilayani Momba.*

# WATUMISHI TSC WATAKIWA KUACHA MIGOGORO NA MIVUTANO KAZINI INAYOKWAMISHA MALENGO YA SERIKALI YA KUTOA HUDUMA BORA KWA WALIMU



*Kikao cha Katibu na Watumishi wa TSC Wilaya ya Momba pamoja na maafisa walioambatana na Katibu huyo kikiwa kinaendelea.*

wao kila kukicha ni migogoro isiyokwisha. Kama ndani ya ofisi hamuelewani ni lazima wateja (walimu) wataathirika, na mimi sipo tayari kuona mwalimu yoyote anapata shida kwa sabau ya watendaji wa ofisi yangu," Nkwama alisema.

Aliendelea kueleza kuwa Ofisi za Wilaya ndiyo moyo wa TSC kwani kwa mujibu wa sheria ndizo zenye mamlaka ya kushughulikia masuala ya Ajira na Maendeleo ya walimu huku zikiwa ni mamlaka ya kushughulikia mashauri ya nidhamu ya walimu pamoja na rufaa za walimu zinazotokana na maamuzi ya mashauri yanayoamuliwa na Wakuu wa Shule.

Kiongozi huyo aliendelea kufafanua kuwa kuwa kutokana na majukumu hayo ambayo mengi yanahusu haki za walimu, watumishi wa TSC wanatakiwa kuwa mfano wa kuigwa, na hivyo wanapaswa kujiepusha na vitendo vyote vinavyokwenda kinyume na maadili ya utumishi wao ikiwemo rushwa.

"Kuna baadhi ya watumishi katika Mkoa huu wa Songwe wanatuhumiwa kwa kutengeneza mazingira ya rushwa kwa walimu. Kama mwalimu amekuja ofisini kwako anahitaji huduma alafu unaanza kumzungusha zungusha lazima atahisi unahitaji atoe chochote ndipo umhudumie. Rais ametuamini na kutupa dhamana hii kubwa, kamwe hatupaswi kwenda kinyume na matarajio na iamni aliyotupa," alisisitiza kiongozi huyo.

Kwa upande wake Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Momba, Juma Seleman alieleza kuwa Wilaya ya Momba ina Halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Momba na Halmashauri ya Mji Tunduma. Wlaya hiyo ina ukubwa wa kilometa za mraba 6275 ambapo kilometa za mraba 5856 ni za Halmashauri ya Wilaya ya Momba na 419 ni za Halmashauri ya Mji Tunduma. Aidha, wilaya hiyo inaundwa na jumla ya Kata 29 ambapo Kata 14 zipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Momba na kata I5 zipo katika Halmashaurj



*Afisa Tawala wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba, Ester Gama akiongea jambo wakati alipomkaribisha Katibu wa TSC pamoja na msafara wake katika ofisi za Halmashauri hiyo hivi karibuni.*

# WATUMISHI TSC WATAKIWA KUACHA MIGOGORO NA MIVUTANO KAZINI INAYOKWAMISHA MALENGO YA SERIKALI YA KUTOA HUDUMA BORA KWA WALIMU

ya Mji Tunduma.

Halmashauri ya Wilaya ya Momba ina jumla shule za msingi 93 zenye walimu 689 na shule za sekondari 14 zenye walimu 201 huku Halmashauri ya Mji Tunduma ikiwa na shule za msingi 49 zenye walimu 507 na shule za sekondari 14 zenye walimu 243 wanaohudumiwa na TSC kwa mujibu wa sheria.

Kuhusu mafanikio ya Ofisi ya TSC Momba katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan, Seleman alisema kuwa ofisi hiyo imefanikiwa kupandisha vyeo walimu 635 ambapo katika idadi hiyo walimu 405 ni wa shule za msingi na 230 ni wa shule za sekondari.

Aliongeza kuwa ofisi yake imepatiwa pikipiki ambayo imekuwa msaada mkubwa katika kusafiri kutoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine pamoja na kufanya ziara mbalimbali shuleni kwa ajili ya kutoa elimu na kutatua kero na malalamiko ya walimu.



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (kulia) akizungumza jambo na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Momba, Juma Seleman (katikati) pamoja na Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia Maadili na Nidhamu ya walimu kutoka TSC Makao Makuu, Robert Lwikolela.*




*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (katikaki) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Momba pamoja na Watumishi wa TSC Makao Makuu mara baada ya kuhitimisha ziara yake wilayani hapo hivi karibuni.*

Alihitimisha kwa kusema kuwa nidhamu ya walimu wilayani hapo inaendelea kuimarika tofauti na siku za nyuma ambapo baadhi yao hususan wanaofanya kazi katika maeneo ya vijijini walikuwa wanajihusisha na ulevi wakati wa saa za kazi kitu ambao kilisababisha ofisi hiyo kuwachukulia hatua za kinidhamu.

Katika ziara hiyo Katibu wa Tume aliambatana na Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia Maadili na Nidhamu ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Robert Lwikolea pamoja na maafisa wengine.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA**
**(TSC)**

# KUMBUKUMBU



**Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli**
**Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

**Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania**,Tunaungana na Watanzania wote katika kumbukizi ya mwaka mmoja wa Kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Hayati Dkt.John Joseph Pombe Magufuli.** Tunatambua mchango wake wa kuwajali na kuwathamini Walimu hadi Serikali kuamua kuanzisha **Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)** nchini ili walimu wahudumiwe kwa ufanisi zaidi.

Tutaendelea kutoa huduma bora ili tutimize maono yake katika usimamizi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu nchini.

**Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania**
**S.L.P: 353 DODOMA**
**Simu: +255 26 2322402**
**Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz**

# ARI YA WALIMU KATIKA UTOAJI TAALUMA WILAYANI MASWA YAIPAISHA SHULE YA MSINGI MWANHEG'ELE HADI NAFASI YA KWANZA KITAIFA KWA SHULE ZA SERIKALI NA NAFASI YA 11 KWA SHULE ZOTE ZA MSINGI NCHINI - TSC MASWA

- **Ushirikiano na ushirikishwaji baina ya wadau wote muhimu yabainika kuwa chachu ya mafanikio;**
- **Kuimarika kwa hali ya nidhamu za walimu kutokana na elimu ya Sheria, kanuni, Taratibu na uzingatiaji wa maadili na miiko ya utendaji kazi;**
- **Utekelezaji wa ahadi za Serikali kwa Walimu ikiwemo upandishaji vyeo, ulipaji wa malimbikizo, n.k;**
- **Walimu kuwajibika ipaswavyo katika utoaji wa taaluma.**

**Na. Mwandishi Wetu – Maswa**

Wakati tukiendelea na maadhimisho ya siku 365 za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Awamu ya Sita, Mama Samia Suluhu Hassan, tangu alipoingia madarakani; Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilayani Maswa, Mkoani Simiyu inayohudumia Halmashauri moja ya Wilaya ya Maswa, inajivunia kwa kiwango kikubwa kuwa sehemu ya mafanikio ya kupaisha elimu wilayani humo hadi kupelekea Shule ya Msingi Mwanheg'ele kuingia katika nafasi ya shule 10 bora Kitaifa kwa shule za Serikali baada ya kuwa Shule ya Kwanza Bora Kitaifa kwa Shule za Serikali na kuwa Shule ya 11 Kitaifa kwa Shule zote za Msingi nchini katika matokeo ya darasa la saba mwaka 2021.



*Kaimu Katibu MSaidizi wa TSC Wilaya ya Maswa, Amon Nhindilo akizungumza na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami katika kikao kilichofanyika wilani hapo hivi karibuni kwa lengo kupata taarifa za utekelezaji wa majukumu ya TSC kwa wilaya hiyo.*

Hilo lilibainika hivi karibuni wakati wa mazungumzo ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami na Kaimu Katibu Msaidizi (KKM) wa TSC - Maswa, Ndg. Amon Nhindilo, wakati wa ziara za kila mwezi za Mkuu huyo wa Mawasiliano ya Serikali na Habari kutembelea Ofisi za TSC Wilaya ikiwa ni sehemu ya mwendelezo wa ziara hizo katika Wilaya 139 zilipo Ofisi za TSC hapa nchini ili kupata taarifa za utekelezaji wa majukumu ya TSC Wilaya pamoja na kutoa elimu zaidi ya uelewa wa majukumu ya TSC kwa wadau muhimu.

"Kwa ushirikiano na ushirikishwaji mkubwa tunaopata kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri hii ya Maswa kwa pamoja na safu nzima ya Uongozi wa Halmashauri hii, zikiwemo Idara ya Elimu Msingi na Sekondari, Ofisi ya Udhibiti Ubora, CWT na wadau wengine muhimu hapa wilayani katika kutoa huduma zetu kama TSC wilaya; tumefanikiwa kwa pamoja kupaisha elimu na kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wetu hadi kupelekea Shule ya Msingi Mwanheg'ele kuingia katika nafasi ya shule 10 bora Kitaifa kwa shule za Serikali baada ya kuwa Shule

# ARI YA WALIMU KATIKA UTOAJI TAALUMA WILAYANI MASWA YAIPAISHA SHULE YA MSINGI MWANHEG'ELE HADI NAFASI YA KWANZA KITAIFA KWA SHULE ZA SERIKALI NA NAFASI YA 11 KWA SHULE ZOTE ZA MSINGI NCHINI - TSC MASWA



*Kikao cha Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Maswa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu kikiwa kinaendelea.*

ya Kwanza Bora Kitaifa kwa Shule za Serikali na kuwa Shule ya 11 Kitaifa kwa Shule zote za Msingi nchini katika matokeo ya darasa la saba mwaka 2021." Alisema Ndg. Nhindilo

Alisema mafanikio hayo yametokana na sababu kadhaa katika utekelezaji wa ahadi za Serikali kwa walimu zikiwemo; kupanda kwa morali na ari ya walimu katika ufundishaji baada ya kupungua kwa malalamiko yanayohusiana na upandaji wa vyeo kwani walimu wanaostahili kupanda hupandishwa kwa wakati kama ilivyofanyika katika kipindi hiki cha mwaka mmoja wa Mama Samia madarakani, lakini pia aliainisha kuwa sababu nyingine ni juhudi kubwa iliyowekwa katika kutoa elimu kwa walimu katika shule zao, kata na tarafa na hivyo walimu kuelimika na kuzingatia maadili na miiko ya utendaji kazi ikiwa ni pamoja na hali ya nidhamu za walimu kuimarika na kuwajibika ipaswavyo katika utoaji wa taaluma.

KKM Nhindilo alisema kuwa pamoja na mafanikio hayo ya kiutekelezaji wa Ilani na majukumu ya Kisheria, bado ofisi yake kwa kushirikiana na Uongozi wa Halmashauri na wadau wengine muhimu wa Kisekta wanaendelea na uhamasishaji wa miiko ya kazi ya ualimu na kutoa elimu kwa walimu wote wanaowahudumia katika halmashauri hiyo kuhusiana na masuala ya Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo, Nguzo za Kazi ya Ualimu, utekelezaji wa zoezi la tathmini ya utendaji kazi yaani OPRAS lakini pia utoaji wa elimu mtambuka kuhusiana na mapambano dhidi ya Rushwa, UVIKO-19, Sensa ya Watu na Makazi 2022, VVU na UKIMWI, athari za madawa ya kulevya na mimba za utotoni kwa wanafunzi.

Akizitaja sehemu ya changamoto pamoja na mafanikio hayo wanayojivunia alikiri baadhi ya shule kutokua na nyumba za kuishi walimu na hivyo kusababisha walimu hao kuishi mbali na vituo vyao vya



*Watumishi wa TSC Wilaya ya Maswa, Kisika Masenyi (wa kwanza kushoto) na Sibu Ndekile wakiwa kwenye kikao.*

# ARI YA WALIMU KATIKA UTOAJI TAALUMA WILAYANI MASWA YAIPAISHA SHULE YA MSINGI MWANHEG'ELE HADI NAFASI YA KWANZA KITAIFA KWA SHULE ZA SERIKALI NA NAFASI YA 11 KWA SHULE ZOTE ZA MSINGI NCHINI - TSC MASWA



*Picha ya pamoja kati ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (wa kwanza kushoto) na watumishi wa TSC Wilaya ya Maswa.*

kazi jambo linalowapa wakati mgumu katika utoaji huduma kwa wanafunzi huku walimu wanaotoka masomoni kuona kama wanapewa adhabu ya kutopandishwa vyeo mara wanaporudi masomoni kwa kigezo cha kutomtumikia mwajiri kwa miaka mine mfululizo awapo masomoni.

Aidha, Afisa Maadili na Nidhamu kwa walimu wilayani hapo Ndg. Kisika Masenyi alisema pamoja na hali ya nidhamu kuendelea kuimarika kutokana na juhudi za TSC katika mwendelezo wa utoaji elimu wilayani humo, kwa kipindi cha utekelezaji wa mwaka wa Fedha 2021/ 2022 unaoendelea kwa robo ya tatu ya mwaka bado hawajapokea shauri hata moja la kinidhamu kutoka kwa Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu wa shule 170 wanazozihudumia ambapo 131 ni Shule za Msingi na 39 ni Shule za Sekondari zenye jumla ya Walimu 1,666 ambapo Walimu 1,112 wanafundisha Shule za Msingi (Wanawake 743 na Wanaume 369) na 554 wanafundisha Shule za Sekondari (Wanawake 91 na Wanaume 463).

Ndg. Masenyi pia alisema mwenendo wa mashauri umeendelea kushuka na kupanda mwaka hadi mwaka akibainisha kuwa juhudi za pamoja za uelimishaji na ufuatiliaji wa walimu vituoni zinaendelea na kuwasilisha taarifa za mashauri katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/ 19 jumla ya mashauri kumi (10) yaliyopokelewa, kushughulikiwa na kuhitimishwa, huku mwaka 2019/ 20 likipokelewa shauri moja (1), mwaka 2020/ 21 mashauri kumi na sita (16) yakiongozwa na utoro na kughushi barua za uhamisho wa vituo vya kazi.

# KATIBU TAWALA, MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA YA ILEJE WAPONGEWA KWA USHIRIKIANO NA TSC

**Na Mwandishi Wetu – Ileje.**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama amewapongeza Katibu Tawala wa Wilaya ya Ileje pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo kwa kufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na Ofisi ya TSC ya Wilaya Hiyo.

Pongezi hizo zimetolewa hivi karibuni wakati Katibu wa TSC alipofanya ziara wilayani Ileje kwa lengo la kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya TSC katika wilaya hiyo ikiwa ni sehemu ya kuazimisha mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan tangu aingie madarakani.

Akiwa katika Ofisi ya Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Nkwama alimshukuru Katibu Tawala huyo kutokana na ushirikiano anaouonesha kwenye ofisi za TSC hususan katika kusadia kutatua changamoto za walimu kitu ambacho kimesaidi TSC kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

"Tunakushukuru Katibu Tawala kwani nimeambiwa kuwa mnatoa ushirikiano wa hali ya juu kwa ofisi yetu, hata hivyo natambua kwamba kwa nafasi yako wewe ni Mjumbe wa Kamati ya TSC. Mmefanya kazi nzuri hasa pale Mhe. Rais Samia Sululu Hassan alipoamua kuwapandisha madaraja walimu, Kamati mlitekeleza wajubu wenu kikamilifu na hakuna mwalimu aliyesahaulika," alisema.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (kushoto) akiongea wakati wa kikao chake na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje kilichofanyika hivi karibuni wakati wa ziara ya Katibu huyo wilayani Ileje.*



*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, Geofrey Nnauye akizungumza wakati wa kikao kati yake na Katibu wa TSC kilichofanyika katika ofisi ya Mkurugenzi huyo hivi karibuni.*

# KATIBU TAWALA, MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA YA ILEJE WAPONGEWA KWA USHIRIKIANO NA TSC



*Kikao cha Katibu wa TSC na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje kikiwa kinaendelea.*

Nkwama alimweleza Katibu Tawala huyo kuwa pamoja na kwamba masuala ya utumishi wa walimu yanakwenda vizuri, bado ipo haja ya kufanya ziara shuleni na kukutana na walimu kuendelea kuwakumbusha juu ya sheria kanuni na taratibu ili kuwasaidia wasiingie kwenye makosa ya kinidhamu.

Sambamba na hilo, Nkwama alimuomba Katibu Tawala huyo kuipatia TSC ofisi katika ofisi za Mkuu wa Wilaya ili watumishi wake waweze kufanya kaazi katika mazingira mazuri kwa kuwa sehemu wanapofanyia kazi wa sasa ni finyu n ani hatarishi kwa afya za watumishi hao.

"Inabidi bado mtusaidia katika kuwafikia walimu, itapendeza kama mkifanya ziara pamoja na wadau wengine wa elimu wa hapa wilayani ili hata walimu wanapouliza maswali, wahusika wote wawepo na kutoa majibu, na kama kuna changamoto kila mtu kwenye eneo lake aweze kuzifanyia kazi kwa haraka. Lakini pia hapa kwenye jengo lako kama kuna nafasi itakuwa vizuri kama mkiwapatia watumishi wetu kwa kuwa mazingira wanayofanyia kazi kwa sasa hayakidhi mahitaji," akisema Nkwama.

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Mathias Mizengo alisema kwamba changamoto ambayo bado wanaiona ni walimu wengi kutaka kuhama kuliko wale wanaotaka kuhamia wilayani hayo, hivyo wana wajibu wa kuona namna ya kuweka mazingira bora zaidi ili walimu wasitamani kuondoka kwenye Wilaya hiyo.

"Walimu wetu wengi bado wanataka kuhama walimu wanaohama ni wengi kuliko wanaokuja. Hapa tuna kazi ya kufanya ili tuhakikisha mazingira yetu yanakuwa rafiki zaidi kwa walimu ili wasitamani kuondoka," alisema.

Alifafanua kuwa ofisi yake imekuwa ikifanya kazi kwa karibu ofisi ya TSC na kupitia ushirikiano huo TSC imeendelea kuwahudumia walimu vizuri na kwa kiasi kikubwa malalamiko ya walimu yamepungua huku akisistiza kuwa Kamati ya TSC wilayani hapo imekuwa ikitenda haki katika masuala yote yanayowahusu walimu.

"Kama mnavyoelewa kazi zetu za Kamati zinahusisha kuamua masuala ya utumishi wa umma wa watumishi wengine, ni kazi

# KATIBU TAWALA, MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA YA ILEJE WAPONGEWA KWA USHIRIKIANO NA TSC

ambayo inahitaji watu waadilifu sana, wasiopenda rushwa wala kumwonea mtu. Kwa kweli mimi na wajumbe wenzangu mara zote tumekuwa tukisimamia sheria katika kutoa uamuzi wa haki kwa walimu," alisema Mizengo.

Aliongeza kuwa, "Tunashukuru ushauri wako juu ya sisi kufanya ziara shuleni kwa kushirikiana na ofisi nyingine zinazoshughulika na elimu, hilo tunalipokea na tutalifanyia kazi mara moja. Unajua kule maeneo ya vijijini baadhi ya walimu wanahisi kama hakuna viongozi, wakati mwingine wanafanya kama wanavyojisikia kitu ambacho sio salama."

Pamoja na hayo Katibu Tawala huyo aliridhia ombi la kuwapatia watumishi wa TSC Wilaya ya Ileje



*Katibu Tawala wa Wilaya ya Ileje, Mathias Mizengo akizungumza na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama wakati katibu wa TSC alipotembelea ofisi ya Katibu Tawala huyo hivi karibuni.*

vyumba vya ofisi katika Ofisi za Mkuu wa Wilaya sehemu ambapo



*Kikao cha Katibu wa TSC na Katibu Tawala wa Wilaya ya Ileje kikiwa kinaendelea.*

# KATIBU TAWALA, MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA YA ILEJE WAPONGEWA KWA USHIRIKIANO NA TSC



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ileje, Deogratias Mhume akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi yake kwa Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (hayupo pichani) wakati wa ziara ya Katibu ya TSC wilayani Ileje iliyofanyika hivi karibuni.*

watafanya kazi katika mazingira bora zaidi.

Kwa Upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Geofrey Nnauye alisema kuwa kwa kipindi cha nyuma Ileje haikuwa iikifanya vizuri sana kwenye masuala ya elimu lakini tayari wameshaandaa mikakati ya namna ya kutatua changamoto zilizokuwa zinakwamisha juhudi za maendeleo ya elimu wilayani hapo.

"Huko nyuma ileje ilikuwa chini kielemu, lakini tumekutana na sekta zote zinazoshughulika na elimu wakiwemo TSC na kwa pamoja tumeandaa mpango mkakati ambao sasa utaifanya Ileje ifanye vizuri zaidi. Kwenye mkakati huo tumetengeneza mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya ziara za pamoja na kupata fursa ya kujadiliana na walimu wetu namna bora ya kuweza kuwahudumia wanafunzi kwa weledi zaidi," alisema Nnauye.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TSC katika Wilaya ya Ileje, Kaimu Katibu wa TSC wa Wilaya hiyo, Deogratias Mhume alianza kwa kueleza kuwa Wilaya hiyo ina jumla ya shule za Msingi 86 na shule za Sekondari 19 za Serikali huku ikiwa na jumla ya walimu 845 ambapo katika idadi hiyo, walimu 549 ni wa shule za msingi na 296 ni wa shule za sekondari.

Mhume alieleza kuwa miongoni mwa mafanikio ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha mwaka mmoja madarakani kwa upande wa Wilaya hiyo ni kuwezesha jumla ya walimu 317 waliostahili kupandishwa madaraja/vyeo kwa mwaka 2020/2021 kupandishwa na kubadilishiwa mishahara yao kwa wakati.

Aliendelea kueleza kuwa, chini ya uongozi wa Rais Samia, elimu na ushauri kwa walimu wenye changamoto za kinidhamu vimetolewa na wengi wao walijirekebisha huku akifafanua kuwa kwa wale ambao hawakujirekebisha hatua za kinidhamu zilichukuliwa dhidi yao.

"Chini ya uingozi wa Rais wetu mpendwa, tumepata fursa kushiriki mafunzo ya uendeshaji wa ofisi hasa yale ya Makatibu Wasaidizi na Wajumbe wa Kamati za Wilaya. Mafunzo hayo yametuongezea weledi katika utendaji wetu wa kazi," alisema.

Aliongeza kuwa "vilevile tunamshukuru Rais Samia kwani chini ya uongozi wake tumepata chombo cha usafiri (Pikipiki-STL 9740). Pikipiki hii imekuwa msaada mkuwa katika kuzifikia shule zetu kirahisi hasa kutokana na jiografia ya Wilaya ya Ileje kuwa na changamoto za kutofikika kwa urahisi," alisema.

Mhume alihitimisha kwa kueleza kuwa, "tuna ushirikiano mzuri baina ya Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya na Ofisi zote za Elimu mfano Idara ya Elimu Msingi, Idara ya Elimu Sekondari, Uthibiti ubora wa Shule na Chama cha Walimu Tanzania (CWT). Aidha, kutokana na ushirikiano mkubwa tunaoupata kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya umetusaidia kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi."

# HEKO SERIKALI KWA JITIHADA MADHUBUTI ZA KUBADILISHA MUUNDO WA UTUMISHI WA WALIMU NCHINI NA UWEZESHAJI WA WARSHA ELEKEZI KWA WALIMU WA AJIRA MPYA NDANI YA SIKU 365 ZA MAMA SAMIA – TSC BARIADI



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Bariadi, Wang'eng'i Mohabe akitoa ufafanuzi juu ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo wakati wa Ziara ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.*

**Na. Mwandishi Wetu – Bariadi**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, imeadhimisha mwaka mmoja wa utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kupongeza na kuunga mkono jitihada madhubuti za Serikali kupitia TSC Makao Makuu za kubadilisha Muundo wa Utumishi wa Walimu nchini, kuridhia kubadilishwa kwa Muundo wa TSC, upandishaji walimu madaraja baada ya baadhi yao kukaa miaka mitano hadi sita bila kupandishwa huku wakiwa na sifa za kupanda tangu mwaka 2016 pamoja na uwezeshaji wa warsha elekezi kwa walimu wa ajira mpya zilizotolewa katika kipindi hicho.

Akizungumza na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka Ofisi za Tume Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, hivi karibuni akiwa ziarani katika mikoa ya Simiyu na Mara, Kaimu Katibu Msaidizi (KKM) wa TSC Bariadi, Ndg. Wang'eng'I Mohabe, alisema; Serikali imefanya kazi kubwa ya utekelezaji wa ahadi na mahitaji muhimu ya walimu ambayo yameongeza tija katika utoaji taaluma kwa wanafunzi ikiwemo ubadilishwaji wa muundo wa utumishi wa walimu na upandishaji walimu madaraja uliositishwa kwa takribani miaka sita iliyopita tangu 2016 jambo lililorudhisha sana nyuma bidii ya walimu katika usimamizi na utoaji huduma hiyo.

KKM Mohabe alisema; "Kwakweli tunajivunia uongozi, utendaji, na utekelezaji wa ahadi za msingi wa Mama Samia kwa walimu wetu tunaowasimamia ambao ndiyo umeleta maarifa zaidi, ari, tija na morali ya uwajibikaji mahali pa kazi, ushirikiano mzuri baina yao na wanafunzi, kupungua kwa kiasi kikubwa kwa malalamiko ya walimu katika nyanja mbalimbali hasa muundo na madaraja, uvumilivu na usikivu katika utumishi wa umma ambao kwasasa unaufanya mkoa wetu wa Simiyu kuwa miongoni mwa mikoa inayofanya vema kitaaluma."

Pamoja na hilo KKM Mohabe alisema TSC Wilaya ya Bariadi inayohudumia Halmashauri mbili yaani Bariadi Mji na Bariadi Wilaya haina shule shikizi hata moja baada ya zote kukamilisha na kupata usajili na hivyo wanahudumia jumla ya shule 169 zikiwa 59 (Msingi 43 na 16 Sekondari) ziko Halmashauri ya Mji wa Bariadi na 110 (Msingi 86 na 24 Sekondari) ziko Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi.

Wakati huohuo KKM Mohabe akiwekea mkazo mwendelezo wa utoaji elimu kwa umma na wateja wanaohudumiwa na ofisi zote za TSC nchini, aliiomba Ofisi ya TSC Makao Makuu kutengeneza na kusambaza katika ofisi zote za wilaya zana za uelimishaji yakiwemo mabango ya kusimamisha, vipeperushi na vijarida ili kutumika kama vielelezo nyakati zote za utoaji elimu kwa umma, wateja na wadau wote muhimu juu ya kazi na majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha TSC.

Vilevile, Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Wilaya ya Bariadi, Ndg. Abraham Maiga, akielezea eneo ambalo wanajivunia katika seksheni ya ajira na maendeleo ya walimu alisema, sehemu kubwa ya walimu wanaohudumiwa na ofisi yao wameweza kujiendeleza



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami akipitia nyaraka zake wakati akiwa katika ofisi za TSC Wilaya ya Bariadi kwa lengo la kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya tume kwa Wialaya hiyo.*

# HEKO SERIKALI KWA JITIHADA MADHUBUTI ZA KUBADILISHA MUUNDO WA UTUMISHI WA WALIMU NCHINI NA UWEZESHAJI WA WARSHA ELEKEZI KWA WALIMU WA AJIRA MPYA NDANI YA SIKU 365 ZA MAMA SAMIA – TSC BARIADI



*Watumishi wa TSC Wilaya ya Bariadi, Abrahamu Maiga (kulia) na Eligiver Kamnde wakipitia baadhi ya nyaraka wakati wa kikao cha Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami (hayupo pichani) kilichofanyika katika ofisi za TSC wilayani hapo hivi karibuni.*



*Afisa Nidhamu wa TSC Wilaya ya Bariadi, Ramadhani Ibrahim akipitia daftari linalohusiana na masuala ya nidhamu ya walimu wakati wa kikao cha Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu kilicho fanyika katika ofisi za TSC Bariadi hivi karibuni.*

kitaaluma kwa ngazi mbalimbali baada ya mwajiri kuridhia kwenda mafunzoni kwa walimu katika nyakati tofauti yakiwemo mafunzo ya muda mrefu na mfupi hivyo kuwa na weledi wa kutosha katika kufuata Sheria, Kanuni, na Taratibu za kazi huku uwajibikaji katika kufundisha ukiongezeka.

Nae Afisa Nidhamu na Maadili ya Walimu kutoka TSC Wilaya ya Bariadi, Ndg. Ramadhani Irunde, akitaja baadhi ya changamoto wanazokabiliana nazo kama ofisi na wanazokabiliana nazo walimu alisema ni pamoja na baadhi ya walimu kuingia katika madeni makubwa yanayopelekea baadhi yao kuwa watoro kazini na wakati mwingine kuacha kazi kabisa, kutokubalika kwa baadhi ya barua za walimu za kupanda madaraja katika mfumo wa mshahara hivyo kukatisha tamaa na kupunguza ufanisi kazini.

Ofisi ya TSC Bariadi inahudumia jumla ya Halmashauri mbili; Halmashauri ya Mji wa Bariadi na Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi zikiwa na jumla ya walimu 2,363 (Halmashauri ya Mji wa Bariadi ikiwa na jumla ya Walimu 995; Msingi walimu 729 ambapo Wanawake ni 400 na 329 ni Wanaume na Sekondari walimu 266 ambapo Wanawake ni 80 na 186 ni Wanaume huku Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi ikiwa na jumla ya walimu 1,368; Msingi walimu 1,061 ambapo Wanawake ni 316 na 745 ni Wanaume na Sekondari walimu 307 ambapo Wanawake ni 65 na 242 ni Wanaume).



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Bariadi. Wa kwanza upande wa kulia ni Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Bariadi, Wang'eng'i Mohabe.*












*Baadhi ya Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika Machi 8, 2022 wilayani Bahi mkoani Dodoma.*

# TSC BUNDA: WALIMU WANA IMANI KUBWA NA UTENDAJI WA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN

**Na Mwandishi Wetu - Bunda**

Mafanikio mbalimbali katika masuala ya utumishi wa walimu yametajwa kuwa moja ya sababu zinazowafanya walimu wilayani Bunda kuendelea kuwa na imani na matumaini makubwa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ikiwa ni mwaka mmoja tangu aingie madarakani.

Magesa Protas, Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Bunda ameyasema hayo hivi karibuni wakati Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami alipofanya ziara katika Ofisi ya TSC Wilaya ya Bunda kwa lengo ya kujua utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo katika kutoa huduma kwa walimu.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Bunda, Magesa Protas (kushoto) akitoa ufafanuzi wa utekelezaji wa majukumu ya ofisi yake kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami katika mahojiano yaliyofanyika hivi karibuni kwenye Ofisi za TSC Bunda hivi karibuni.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami (kulia) akizungumzo na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Magesa Protas katika Ofisi za TSC Bunda hivi karibuni.*

Magesa alianza kwa kueleza kuwa Ofisi ya TSC Bunda inahudumia Halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Bunda (Bunda DC) na Halmashauri ya Mji Bunda (Bunda TC) ambapo Bunda DC ina jumla ya shule za Serikali 124 zenye walimu 1,222 huku Bunda TC ikiwa na shule za Serikali 80 zenye walimu 1,080 wa Msingi na Sekondari.

Ofisi hiyo imebainisha kuwa Rais Samia Suluhu Hassan amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuendelea kujenga imani na matumaini kwa watumishi wa Umma wakiwemo walimu wilayani hapo kutokana na

# TSC BUNDA: WALIMU WANA IMANI KUBWA NA UTENDAJI WA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN



*Afisa TSC Wilaya ya Bunda anayeshughulikia masuala ya Nidhamu na Maadili ya Walimu, Charles Bisansaba akiwa anaendelea kutekeleza majukumu yake ofisini kwake.*

kufanya mambo makubwa ambayo yameondoa kero, malalamiko na kuongeza morali ya utendaji wa kazi.

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ilipandisha vyeo jumla ya walimu 872 ambapo katika idadi hiyo walimu 646 ni wa shule za msingi na 226 ni wa shule za sekondari huku jumla ya walimu 51 (41 wa shule za msingi na 10 wa shule za sekondari) wakibadilishiwa kazi/cheo baada ya kujiendeleza kielimu.

Kwa upande wa Halmashauri ya Mji Bunda, jumla ya walimu 618 walipandishwa vyeo, katika idadi hiyo walimu 414 ni wa shule za msingi na walimu 204 ni wa shule za sekondari huku jumla ya walimu 52 (33 kutoka shule za Msingi na 19 wa shule za sekondari) wakibadilishiwa kazi/cheo.

Akielezea namna zoezi la upandishaji vyeo/madaraja walimu lilivyofanyika katika wilaya hiyo, Magesa alisema kuwa tofauti na miaka ya nyuma ambapo zoezi kama hilo lilikuwa linachukua muda mrefu kukamilika, Rais Samia Suluhu Hassan aliwashangaza wengi kwa kulifanya zoezi hilo kukamilika kwa ufanisi na kwa muda mfupi jambo ambalo limeleta faraja kwa walimu.

"Zoezi la kuwapandisha vyeo walimu lilifanyika kwa muda mfupi sana kitu ambacho tulikuwa hatujahi kufikiria kama kinawezekana. Kwa kweli tulifanya kazi usiku na mchana kuhakikisha tunakamilisha zoezi hilo ndani ya muda uliokuwa umewekwa. Walimu wamefarijika sana kwa kuwa hichi kilikuwa kilio chao cha muda mrefu lakini sasa Rais wetu amewafuta chachozi," alisema Magesa.

Akiendelea kuzungumzia zoezi hilo, Magesa alisema kuwa kwa miaka ya nyuma ilikuwa inachukua muda mrefu kutoka mwalimu anapopandishwa cheo hadi kuanza kupokea mshahara wa cheo kipya, lakini katika kipindi cha Rais Samia upandishaji wa vyeo umekwenda pamoja na mabadiliko ya mishahara kitu ambacho kimeondoa madai ya malimbikizo ya mishahara kwa walimu.

"Huko nyuma ili kuwa inachukua muda mrefu walimu kupata mishahara mipya kitu ambacho kilisababisha walimu kuwa na madai ya muda mrefu ambapo hadi sasa wapo ambao bado hawajalipwa. Hata hivyo, tunamshukuru Rais kwa kuwa walimu wameendelea kulipwa madai yao, hata hao waliobaki tunaamini nao watalipwa hivi karibuni. Katika zoezi hili la mwezi Juni 2021, mishahara ya walimu ilibalilishwa mapema sana, tunampongeza Mama Samia kwa mafanikio hayo ambayo yameondoa kero ya malimbikizo ya madeni," alisema Magesa.

Magesa aliongeza kuwa, Rais Samia Suluhu Hassan amewaheshimisha walimu kwa kuwafanya watekeleze majukumu yao katika mazingira bora baada ya kufanya kazi kubwa ya kuboresha miundombinu ya shule nchi nzima ikiwemo ujenzi wa vyumba vya madarasa kitu ambacho kimewafanya walimu waone kuwa Rais anathamini mazingira yao ya kufanyia kazi.

Kiongozi huyo aliongeza

# TSC BUNDA: WALIMU WANA IMANI KUBWA NA UTENDAJI WA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN

kuwa kutokana na Rais Samia Suluhu Hassan kushughulikia masuala ya watumishi wa umma, walimu wilayani hapo wamekuwa mstari wa mbele katika kufanya kazi kwa bidii na hata hali ya nidhamu imeendelea kuwa nzuri ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

"Ninachoweza kusama ni kuwa walimu wa Bunda wamebadilika kwa kiasi kikubwa, mashauri ya nidhamu yamepungua kutoka 46 mwaka 2016/2017 hadi 8 mwaka 2020/2021 na kwa mwaka huu yameendelea kupungua zaidi. Tunaamini moja ya sababu zinazofanya walimu waendelee kuwa bora ni jitihada za Rais katika kutatua changamoto zinazowakabili," alisema.

Pamoja na hayo, Magesa anashauri kuwa ili kuendelea kutoa huduma bora zaidi kwa walimu, Ofisi ya Mkurugezi wa Bunda TC na Bunda DC zinapaswa kuongeza ushirikiano na TSC hususani katika masula ya kuandaa bajeti ya mishahara ya walimu (PE) ili kuhakikisha kila mwalimu anatendewa haki katika utumishi wake kama taratibu zinavyelekeza.

Vilevile, alieleza kuwa kumekuwa na tabia ya walimu kukopa kupita kiasi kitu ambacho kimesababisha wengi wao kuwa na msongo wa mawazo na kuondoka katika vituo vyao vya kazi ili kuwakimbia wanaowadai kitu ambacho kimesababisha ofisi yake kuwachukulia hatua za kinidhamu ambapo baadhi yao wamejikuta wakikabiliana na adhabu mbalimbali ikiwemo kufukuzwa kazi.

Alihitimisha kwa kutoa wito kwa jamii ya Wilaya hiyo kutoa ushirikiano kwa walimu waliopo kwenye maeneo yao ili waweze kuwahudumia watoto wao vizuri badala ya kuwafanyia vitendo vya kishirikina ambavyo vimekuwa vikisababisha walimu kukata tamaa ya kufanya kazi katika wilaya hiyo.



*Picha ya Pamoja kati ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (katikati), Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Bunda, Magesa Protas (kushoto) pamoja na Afisa anayeshughulikia Maadili na Nidhamu ya Walimu wa Wilaya ya Bunda, Charles Bisansaba.*

# KESI ZA UTORO WA WALIMU KATIKA VITUO VYA KAZI WILAYANI MUSOMA ZAONGOZA KULIKO MAKOSA MENGINE YA NIDHAMU HUKU WALIMU WA KIUME WAKIWA VINARA KWENYE UTORO

**Na. Mwandishi Wetu – Musoma**

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa hivi karibuni na Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) – Musoma inayohudumia walimu wanaotoa huduma ya taaluma katika shule za Manispaa ya Musoma na Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, imebainika kuwa kesi za utoro wa walimu katika vituo vya kazi ndizo zinazoongoza kuliko makosa mengine ya kinidhamu huku walimu wa kiume wakionekana vinara kwenye utoro.

Imeelezwa kuwa kutokana na hali hiyo katika jitahada za kupunguza mashauri ya kinidhamu yanayotokana kwa sehemu kubwa na tatizo la utoro ofisi hiyo ya TSC wilayani Musoma inaendelea kuwatembelea walimu katika vituo vyao vya kazi ili kutoa elimu juu ya Sheria, Kanuni, Taratibu, na Miongozo mbalimbali ya utendaji kazi kwa watumishi wa umma, kuwakumbusha na kuwasihi juu ya athari za makosa ya kinidhamu katika utumishi na kuwakumbusha kuhusiana na adhabu za makosa mbalimbali yakiwemo ya nidhamu na maadili kazini lengo likiwa ni kuongeza ufanisi zaidi wa utendaji kazi kwa mwalimu.

Akizungumza hivi karibuni na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka Ofisi za Tume Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, akiwa ziarani katika mikoa ya Simiyu na Mara; kwa niaba ya Kaimu Katibu Msaidizi (KKM) wa TSC Musoma, Ndg. Samwel Biyan, Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka Ofisi ya TSC – Musoma Mwl. Richard Msema, alisema; hali ya nidhamu wilayani hapo imekua ikibadilika mwaka hadi mwaka ambapo kwa mwaka 2017/ 18 jumla ya mashauri ya nidhamu 12 yaliwasilishwa na kufanyiwa kazi ambapo kati ya hayo sita yalitokea Manispaa ya Musoma na sita mengine yalitokea Halmashauri ya Wilaya ya Musoma kwa uwiano wa msingi mawili na sekondari 10 kwa wilaya nzima kattika mwaka huo.

Afisa Ajira huyo na Maendeleo ya Walimu aliongeza kuwa katika mwaka 2018/ 19 hali ya nidhamu ilibadilika kwani jumla ya mashauri ya nidhamu 78 yaliwasilishwa na kufanyiwa kazi ambapo kati ya hayo mashauri 76 kutoka Manispaa ya Musoma na Halmashauri ya Wilaya ya Musoma yalitokana na vyeti feki kwa Shule za Msingi 74 na Sekondari mawili huku mawili yakitokana na ukaidi, na kuajiriwa bila sifa.

Vilevile Afisa Ajira huyo na Maendeleo ya Walimu Mwl. Msema alisema katika miaka iliyofuata hadi kufikia mwaka 2021/ 22 ambao tayari wamepokea mashauri matano kwa halmashauri zote mbili, hali iliendelea kubadilika ambapo mwaka 2019/ 20 walipokea jumla ya mashauri ya nidhamu 18, mwaka 2020/ 21 mashauri 20 yaliyopelekea



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami akiongea na Watumishi wa TSC Wilaya ya Musoma (hawapo pichani) wakati wa ziara yake aliyoifanya wilayni hapo hivi karibuni.*



*Afisa Maadili na Nidhamu wa TSC Musoma, Mhoja Tanganyika John akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wilaya hiyo kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani). Aliwasilisha taarifa hiyo kwa niaba ya Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Musoma ambaye alikuwa na majukumu mengine nje ya ofisi wakati wa ziaraya ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali iliyofanyika hivi karibuni.*

# KESI ZA UTORO WA WALIMU KATIKA VITUO VYA KAZI WILAYANI MUSOMA ZAONGOZA KULIKO MAKOSA MENGINE YA NIDHAMU HUKU WALIMU WA KIUME WAKIWA VINARA KWENYE UTORO




*Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC Musoma, Richard Msema akitoa ufafanuzi wa utekelezaji wa majukumu ya TSC wakati wa ziara ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu iliyofanyika wilayani hapo hivi karibuni.*




*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (wa kwanza kulia) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Musoma.*

jumla ya miaka yote kuanzia mwaka 2017/ 18 mpaka 2021/ 22 kuwa na jumla ya mashauri 133 ya nidhamu ambapo 56 yalitokea Manispaa ya Musoma (44 Shule za Msingi na 12 Sekondari) huku 77 yakitokea Halmashauri ya Wilaya ya Musoma (63 Shule za Msingi na 14 Sekondari); Wanawake wakiwa na uwiano wa jumla ya mashauri 65 kati ya jumla ya mashauri yote 133 na Wanaume wakiwa vinara kwa mashauri 68 ya mashauri yote.

Alitaja baadhi ya mambo ya kujivunia wilayani humo kutoka kwa walimu wanaowasimamia kuwa ni pamoja na kupungua kwa malalamiko yaliyohusiana na maslahi yao baada ya Serikali kufanya malipo ya malimbikizo na kulipwa kwa mishahara mipya baada ya walimu kupandishwa madaraja, kubadilishiwa kwa muundo wa utumishi wa walimu, kuimarika kwa uhusiano mwema kikazi kati ya Ofisi ya TSC na walimu na kushirikiana na walimu kwenye vikao mbalimbali vya Kisekta na semina kufanyika kwa walimu ili kuimarishana, kuongeza weledi na kujengeana uwezo zaidi katika utoaji wa taaluma kwa wanafunzi.

Mwl. Msema alisema pamoja na mambo hayo machache ya kujivunia wilayani humo, kuna changamoto wanazokabiliana nazo ikiwemo uhaba wa nyumba za walimu shuleni, umbali kutoka kwenye makazi ya walimu hadi kwenye vituo vya kazi, visa vya kimazingara ikiwemo uchawi, wizi, mauaji n.k, waajiri kuwapangia majukumu tofauti na taaluma zao, Ofisi ya TSC kutoshirikishwa na mwajiri katika mazoezi mbalimbali likiwemo la kuhamisha walimu, kuandaa mpango wa mafunzo kwa walimu, uhaba wa samani, na usafiri wa ofisi usiokidhi mahitaji kulingana na jiografia na miundombinu ya wilaya wanayoihudumia.

Ofisi ya TSC Wilayani Musoma, Mkoani Mara inahudumia Halmashauri mbili ambazo ni Manispaa ya Musoma na Halmashauri ya Wilaya ya Musoma zikiwa na jumla ya shule 191 ambapo 58 ziko Manispaa ya Musoma (40 Shule za Msingi na 18 za Sekondari) huku 133 zikiwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Musoma (111 Shule za Msingi na 22 Sekondari), zikihudumiwa na jumla ya Walimu 2,390 ambao kati ya hao 1,109 wanahudumu katika Manispaa ya Musoma ikiwa ni walimu 689 wa Shule za Msingi (425 Wanawake na Wanaume 264) na Walimu 420 wa Shule za Sekondari (153 Wanawake na Wanaume 267). Vilevile inahudumia jumla ya Walimu 1,281 katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma ambao kati yao 976 wanafundisha Shule za Msingi (Wanawake 381 na Wanaume 595), na Walimu 305 wa Shule za Sekondari (69 Wanawake na Wanaume 236).

# MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN UMEKUWA WA NEEMA KWA WALIMU BUTIAMA




*Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Butiama anayeshughulikia Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu, Regina Donatus Kinabo akiwa ofisini kwake.*

**Na Mwandishi Wetu - Butiama**

Wakati mafanikio ya utendaji wa kazi wa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan yakionekana katika sekta mbalimbali ikiwa ni mwaka mmoja tangu aingie madarakani, Ofisi ya TSC Wilaya ya Butiama imekiri kuimarika kwa nidhamu, kuongezeka kwa morali ya kazi na kupungua kwa malalamiko kwa walimu wa wilaya hiyo.

Mafanikio hayo yamepatikana kutokana na juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan za kuinua sekta ya elimu ikiwa ni pamoja na kuboresha utumishi wa walimu huku lengo kubwa likiwa ni kuhakikisha walimu wanakuwa na mazingira bora ya kazi ili waweze kutoa huduma bora ya kufundisha wanafunzi.

Regina Donatus Kinabo ni Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) anayeshughulikia masuala ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu katika Wilaya ya Butiama ambaye alifanya mahojiano na Jarida hili kwa niaba ya Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC wa wilaya hiyo ambapo alibainisha mafanikio mbalimbali yaliyopatikana kutokana na utendaji kazi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan.

Kinabo alianza kwa kueleza kuwa, walimu wote waliokuwa na sifa za kupanda vyeo/madaraji katika wilaya hiyo walipandishwa kwa asilimia 100 kitu ambacho hakikuwahi kutokea katia utumishi wa walimu katika miaka ya hivi karibuni.




*Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Butiama anayeshughulikia Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu, Regina Donatus Kinabo akitoa ufafanuzi wakati wa mahojiano na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami yaliyofanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC Butiama.*

# MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN UMEKUWA WA NEEMA KWA WALIMU BUTIAMA



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami akizungumza na Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Butiama anayeshughulikia Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu, Regina Donatus Kinabo katika mahojiano yaliyofanyika hivi karibuni wilayani Butiama.*

"Hatujawahi kushuhudia upandishaji wa madaraja ukifanyika kwa mafanikio kama ule wa mwezi Juni 2021. Huko nyuma tulikuwa na changamoto sana kwenye eneo hili, kwa mfano katika zoezi la upandishaji madaraja la mwaka 2019 walimu waliokuwa na sifa za kupandishwa walikuwa 399 lakini ikama ilikuwa na nafasi 57 tu, hivyo walimu 342 hawakupandishwa pamoja na kwamba walikuwa na sifa," alisema Kinabo.

Afisa huyo alifafanua kuwa katika zoezi la upandishaji vyeo lililofanyika katika mwaka wa fedha 2020/2021 chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, TSC Butiama ilipandisha walimu 641 wa Shule za Msingi na walimu 265 wa Shule za Sekondari na kufanya jumla ya walimu waliopanda madaraja kwa mwaka huo kuwa 906 ambapo idadi hiyo ilihusisha walimu 399 ambao hawakupandishwa mwaka 2019.

Tofauti na siku za nyuma, Ofisi ya TSC Wilaya ya Butiama ilifanikiwa kuwabadilishia kazi/cheo walimu 151 ambao ndio waliowasilisha maombi ya kubadilishiwa kazi/cheo baada ya kujiendeleza kimasomo na kukidhi vigezo vingine vya kufanyiwa mabadiliko hayo kwa mujibu wa Sheria Kanuni na Taratibu za Tume ya Utumishi wa Walimu.

"Tunamshukuru Rais wetu kwa kuendelea kuwajali walimu kwani baada ya zoezi la upandishaji wa madaraja kukamilika aliruhusu walimu wenye sifa kubadilishiwa kazi/cheo. Hii ilisaidia sana kuleta utulivu kwa walimu wetu kwani kulikuwa na wimbi kubwa la walimu waliokuwa wanahitaji kufanyiwa mabadiliko hayo kwa muda mrefu bila mafanikio," alisema Kinabo.

Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Ofisi hiyo imeendelea kushughulikia vibali vya kustaafu kazi ya ualimu ambapo imetoa vibali kwa walimu 15, katika idadi hiyo walimu 3 wanastaafu kwa hiari na walimu 12 wanastaafu kwa lazima baadi ya kufikia ukomo wa utumishi wao kwa

# MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN UMEKUWA WA NEEMA KWA WALIMU BUTIAMA

mujibu wa sheria.

"Tumeendelea kuwashughulikia walimu wanaostaafu kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa nyaraka zao zipo vizuri na kuwapatia vibali kwa wakati ili kuwaepushia usumbufu katika kushughulikia mafao yao. Tunashukuru kwani tumeendelea kutekeleza jukumu hili kwa weledi na hata walimu wanapowasilisha nyaraka zao kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wamekuwa wakipata mafao yao ndani ya muda mfupi tofauti na zamani," alisema.

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan akiwa madarakani ofisi hiyo imefanikiwa kuendelea kuwafikia walimu katika maeneo yao na kutoa elimu juu ya masuala ya mbalimbali ya utumishi wao kitu ambacho kimesaidia kuimrika kwa nidhamu na kupungua kwa mashauri ya nidhamu ya walimu.

"Tumefanikiwa kutembelea shule 31 za Msingi na Sekondari, tumefanya kikao na Wakuu wa Shule 88 na Shule Shikizi 5 pamoja na Maafisa Elimu Kata 18. Tumezungumzia masuala ya Maadili ya Kazi ya Ualimu na kuhakikisha kila mwalimu anapata nakala ya kijitabu cha masuala hayo. Pia tumewakumbusha Wakuu wa Shule wajibu wao wakiwa ni mamlaka ya kwanza ya nidhamu kwa walimu pamoja na namna ya kuandaa hati ya mashtaka na notisi. Vilevile, tumewafunsisha walimu taratibu na namna ya kukata rufaa pale inapotokea hawajaridhika na uamuzi ya shauri la nidhamu," alisema.

Alihitimisha kwa kueleza kuwa mashauri ya nidhamu yamepungua kutoka 23 mwaka 2017/2018 hadi shauri 1 mwaka 2021/2022 na hivyo kufanya walimu kuongeza kasi ya uwajibikaji na kuifanya Wilaya hiyo kuendelea kuongeza kiwango cha ufaulu katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo na kufanikiwa kupata Tuzo za Ubora wa Taaluma kwa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita zilizotolewa hivi karibuni.




*Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Butiama anayeshughulikia Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu, Regina Donatus Kinabo akimsikiliza Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami wakati wa mahojiano yaliyofanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC Butiama.*



**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
**Simu:** +255 (26) 2322402-4 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz* **Tovuti:** *www.tsc.go.tz*

*Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania* *tumeyautumishiwawalimutanzania*